Neno la wasomaji

Viongozi wa chama cha MPR hawaelewi si asa ya nchi

Tangu mageuzi ya siasa yakubaliwe rasmi nchini Zaire, bada ya upinzani mkali wa wanainchi, mambo na kelele hayakomi kwa wanasiasa wa MPR. Viongozi hao wasema mengi sababu wa jua siku zao ni arubaini (40) sasa na woga wawashika.Madaraka waliopata tangu hapo nchi yetu kajichukulia uhuru yafikia mwisho. Na hii ndio tishio kubwa sana kwao sababu walipotawala hakuna hata aliyewastusha, ila kwa sasa mambo yapinduka. Baada ya sehemu hiyo ya kwanza, aina ya pili ni watu wasio na madaraka ila wapendelevu wa chama ambao wapata chakula chao bila kukichokea. Hivyo walinda mahitaji na mafundisho ya wakubwa wao vigogo, madikteta wakisahau kama kinacho mwanzo lazima kiwe na mwisho. Kundi la tatu ni lile la mashabiki, watu wanaopiga kelele ambao kwa hakika hawajui wanachokifanya. Hao ni bendera ifuatayo upepo punde wajielekeza, hawapati lolote ila wanaweza kutumiwa katika vurugo wakati wapinzani wajitahidi kulihotubia umma.Vikundi hivyo vitatu vifahamu kuwa vyakabiliwa na shida na matatizo na muda huu ni mgumu sana kwao. Wajue kama mfumo wa demokrasia wapamba moto ulimwenguni kote. Na ni sherti uinuke kabisa bila hofu.

Faraja miongoni mwa raia ni kuona watu wachukia sana siasa ya chama kimoja na wote wapendelea mabadiliko. Hii ndio taa iwaangaziao raia na kutupilia mbali mauaji, zulumu, vitisho na kazalika. Kufikia demokrasia, sherti njia ndefu ipitiliwe. Leo hii, sisi ni matunda ya historia ya babu zetu, na kwa nini kugandamizwa wakati tumekwisha kuwa huru ? Labda tungesema ni vema kuwa chini ya utawala wa wakoloni, wakati sisi kwa sisi hatujipatie amani (mfano wa miaka 28 ya utawala wa Mobutu) na hatupendi kukanusha makosa ya viongozi kwa woga ya kuwekwa gorogoroni ? Viongozi hao, wajionesha kuwa wapo weupe moyoni na rohoni, hawana zambi wala uchafu, wafanya mema na kujua yote. Kuwaonya makosa yao, eti ni kukosa adabu. Je ! hayo ni kweli ?

Mengi mema wasemayo kafanya, yako wapi ? Falsafa hii potovu ya kujiaminia yapatikana miongoni mwa watu wengi nchini Kongo (Zaire).

Kwa oni langu, ningependelea raia wa Kongo kusimama imara nyuma ya nguzo ya demokrasia na kujua kama ushindi na ushujaa ni wetu. Tabia waliojenga na kuwaza sisi raia ni watumwa, watumishi wao yaweza kutuamrisha, na wazani ya kuwa tabia hiyo haijatoka akilini mwetu.

Kumbe wajindanganya. Kwa sababu walijipandikiza madarakani kwa kutumia njia potovu, hao waofu zambi waliotenda na kuogopa eti yatawakwama kooni siku moja. Ni lazima wawajibike kwetu sisi raia wa nchi hii safi, nzuri ya maziwa na asali. Kuona twaishi si kwa udikteta wala kwa siasa yote bali kwa neema ya Mungu, twaendelea kupumua wakati taabu yapita kipimo. Mungu abariki nchi yetu ne viongozi wa mageuzi. Barikí Kongo mpya.

Msomaji
Omari Mtange wa Mtange
Baraka centre Fizi

***NLU** : Msomaji wetu Mtange unayoyatoa ni maoni yako mwenyewe. Na labda kunayo ukweli. Ila wanachama wote wa MPR hakuna hata lolote kafanya kuwa kweli njema ?*

Afya

Sherti wanaozalisha waelimishwe

Wamama wanaozalisha kwa njia ya kiasili wafanya kazi njema vijijini ~~~rani Afrika. Kitendo hicho chatokana na kitambo cha mahali wakaapo na hospitali, malipo ya matibabu na mara wamama wengi vijijini hawajui wakati wao wa kuzaa, ni sherti wajifungue manyumbani kwao. Mara desturi na mila zafunga wengi vijijini ili wasijielekeze kwenye hospitali sababu ya matatizo kaweza katokee, wasemavyo. Hapo wanaozalisha waonekana kuwa na kazi muhimu ya kuwasaidia wamama wale. Ila miongoni mwao wakosa ujuzi fulani fulani na vifaa kazaa kwa kuheshimisha huduma yao. Huenda vitofu vya watoto wazaliwa vyakatwa na vitu visivyoaminiwa na mahali pasipo kweli nzuri. hayo yote yaweza kuwa chanzo cha magonjwa ya mtoto hata atakapokuwa mtu mzima. Kuona jambo hilo lafanyika labda mahali pote vijijini mwa Afrika, mipango rasmi yaanza kuchukuliwa ili kazi hiyo ikubaliwe hata na serkali ila kwa shurti zimoja.

Huko nchini Togo, kwa mfano yapata akina mama 10 wanaozalisha kwa njia ya kiasili wa jimbo la Kozah, kafunzwa yapata juma tatu hivi. Somo lao kaelekea kujua shurti za misingi ya afya : kuosha mikono, usafi wa mahali wazalishapo na kazalika. Ikiwa mafundisho kafanywa na walimu wao, maelimisho kwa vitendo kafanyika kunako hospitali ya Kara. Huko waganga kawasukuma wanafunzi wale kujua namna ya kutumia njia za kisasa za uzalishaji, kama vile kuchungua mimba, kujua hasara yanayoweza kutokea, kuchanjwa ndui kwa bibi mja mzito, kujua kuzalisha na kuokoa bibi wakati wa hatari, namna ya kutunza mtoto na mamae, kushurulikia watoto wanaokabiliwa na shida, shauri ya malisho na kwa upangaji wa uzazi, namna ya kutumia vyombo vya uzazi na kazalika.

Wanafunzi hao kapewa vifaa vitakavyo wasukuma kutokusahau yale waliofunzwa. Adibisho hilo ni hatua ya kwanza kwa mradi moja kutolewa pesa na shirika la UNICEF na ambalo latezamia kuelimisha watu yapata 50 wahusikao jimboni mwa Kara. Ni mfano bora ambao waweza kuigwa na wamama wengine pia mashirika yahusikayo, ili wapate kiwango cha ujuzi kwa ajili ya kazi yao na kuokoa maisha ya mama na mtoto. Na ni kwa kusudi lile moja, mkutano na akina mama wajuzi "sages femmes" wa dini la kibahai mjini Bukavu kaendeshwa hapo majuzi kwa kukamilisha huduma yao. Kumbe ni vema maelimisho hayo yafanywe mahali mengi kwa kufikia mahitaji ya maendeleo.

Mutungwa Abandelwa
Phély

JE, UMESIKIA ...

Kuwa
Wanafunzi wa chuo cha maelimisho ya ufundi hapo majuzi kamuendea arkiaskofu wa dini la kikatoliki mjini Bukavu na kumuomba amuondoe madarakani padri kiongozi wa chuo hicho "ITFM" ? Yasemekana huko eti padri huyo pahali pa kuchungua kwa karibu kazi za uongozi wa chuo, huyo kajiruhusu kuheshimia zaidi kinywaji na ... Eti pia katumia feza toka mavuno ya vyombo, vitu vyatengenezwa na wanafunzi kwa njia ajua mwenyewe pahali pa kuuza vifaa kazaa kwa maelimisho bora ya wanafunzi. Bila kusahau kuuzishwa kwa vingine vifaa kaachwa na Mafrera "Maristes". Sisi hatuhukumu padri huyo na wakuu wake waliomkabizi madaraka hayo na ambao kwa nia wajua wenyewe kawanyanganya mafrera hao uongozi wa shule hilo. Ila ni wanafunzi, na wengineo wanaohusika kaandamana kwa kupinga hatua kachukuliwa. Basi kati ya padri na wafuasi wake nani kaombeshwa toba ?

Kama
haufanye angalisho waweza kutimuliwa na vikundi vya warugaruga na wengineo wizi kazaa ambao watangatanga kama mbwa mwitu mjini wakitafuta vitovero ? Yatezamiwa kuwa mjini wayangunyangu hao wamekwisha kuwateka nyara wakaaji wengi wakiwadanganya eti wana biashara kazaa kama vile vyakula mchele, maharangi na kazalika wakiomba tu feza za kulipa usafirishaji wa bizaa hiyo. Hapo majuzi ni mfundi moja mshonaji na mtu mwengine wa kazi katika shirika moja mjini katishwa. Kwa bahati nzuri mwizi huyo siku hiyo ilikuwa kwake ya arubaini kwa kuwa kashikwa na kutupwa gorogoroni ambako ajuta makosa yake. Lakini ni kwa muda wa siku ngapi ?

Kwamba
vijana wamoja katika mtaa wa Bagira na hakika katika mikoa midogo ya Fariala na Nyamuhinga kaonya haya kwa mama moja na mtoto wake ?

Tega sikio. Katika mpango wa kuwasaka walozi, vijana hao wa Bagira wakihimizwa na kusukumwa na wazazi na majirani kashika gongo, visu na ziinginezo silaha, kuwatukana na kuwavua nguo akina mama Kasiba na bintiye wakisagwa vikali makonde, kupigwa kama nyoka na hiyo mbele ya mapadri na waumini wa kanisa katoliki, eti ni walozi. Yajulishwa huko eti akina mama hao kajionea cha mtema kuni. Kweli cha mtema kuni kwani walilazimishwa kujioga katika maji kabarikiwa na kunyweshwa kinywaji kikali kama sigi na bila hata mtu moja kama vile mapadri na viongozi na wote wa naohusika na usalama kuja kuwaondoa mikononi mwa watenda maovu hao.

Eti
jimbo la Kivu ya Kusini haliangamizwe tu na uchafu kutupwa mahali kazaa, matatizo ya afia, ya kupinga magonjwa ya kuhara na mengineo ya kuambukiza kama vile kisonono, na mengineo ya haya ? Hapo siku zilizopita mtaani Uvira kunako mipaka ya nchi ya Zaire na Burundi hapo Kavimvira, kashikwa mchuuzi moja wadawa ambaye kajiruhusu bila woga kuchukua nchini kiasi kikubwa cha dawa zilizoharibika. Dawa hizo toka nchi jirani ya Burundi zilikuwazikipelekwa mjini Bukavu na kandokando. Kuambatana na maelezo ya mhuni huyo Shimba ambaye kakamatwa na wafanyakazi wa "OZAC" ambao wahusika na uchunguzi wa biashara vyaingizwa nchini kama ni vizuri ao vibaya, dawa hizo sizo za kwanza kwani ni tangu siku nyingi zaidi ya miaka kumi zaingizwa nchini na kutolewa kwa wagonjwa. Yajulishwa kuwa dawa hizo zaogotwa kwenyi yarara za gala, maduka ya dawa ama "pharmacies" na mahospitali nchini Tanzania na Burundi. Wachuuzi wa dawa hizo wabadilisha tarehe na siku za kuisha nguvu ama za kuharibika na kuziuzisha kwa bei chini kunako soko za mtaa wa Uvira, mjini Bukavu hasa Kadutu na kandokando. Hum ! Na hapo makesho husema kuwa magonjwa ya haya na mengineo ya kuhara hayaponi jimboni mwa Kivu ya Kusini. Loo !

Kuwa
kikundi cha ndugu wanaohitaji mji wa Bukavu urudishiwe uzuri wake ama wa "Ecolos" kapinga kabisa uharibifu wa mji usiendelee siku nenda rudi ?

Kwa kweli mji wa Bukavu ambao kasifiwa kwa uzuri wake na kuwavuta watalii wengi na kuingiza feza nyingi za kigeni kwa manufaa ya serkali na raia hapo siku zilizopita leo hii umeharibika ajabu. Hasa kutokana na kukatwa kwa miti na ujenzi ovyo ovyo mjini. Vitendo ambavyo vyaendeshwa na wakuu na wafanyakazi wa serkali mahali kazaa wakiruhusu mambo hayastahili kwa kuulinda mji ubaki kisasa. Kikundi hicho baada ya kukasirika kamweendea mtu mmoja ambaye hatutataja jina lake na kumlazimisha avunje haraka pango kasimika kwenyi kiwanja ataka kujenga hapo pembeni ya jela kubwa la Bukavu. Kwa sasa huyu ajitahidi kuwabembeleza lakini hawa waziba masikio. Uzuri wa mji ndiyo shuruli lao.